


KOMESHA

UKEKETAJI



Ukeketaji ni nini?

Ukeketaji inamaanisha “female genital mutilation” yaani “ukeketaji”.



Jua ukweli

Ukeketaji inajumuisha njia zote zinazohusisha kukata na kutoa sehemu ya uchi wa mwanamke au msichana ama kukata na kutoa uchi wote wa mwanamke au msichana. Pia inahusisha madhara mengine kwa uchi wa mwanamke au msichana ama utaratibu wowote unaodhuru uchi wa mwanamke au msichana, kwa sababu zisizo za kimatibabu.

Utaratibu huu hauna faida za kiafya kwa wasichana na wanawake na unaweza kusababisha madhara mengi kwa mwili wao.

Ukeketaji inafanywa mara nyingi kwa wasichana wadogo wenye umri wa kati ya mwaka mmoja hadi 15.

Zaidi ya wasichana na wanawake milioni 125 wamekeketwa katika nchi 29 zilizoko Afrika na Mashariki ya Kati ambapo Ukeketaji inatekelezwa.

Ukeketaji ni ukiukaji wa haki za binadamu ya wasichana na wanawake.

Ukeketaji ni haramu nchini Kenya. Asilimia 27 ya wasichana na wanawake wamekeketwa humu nchini.

Athari za kiafya – za muda mfupi

Ukeketaji haina faida zozote za kiafya , na ni hatari kwa wasichana na wanawake . Inahusisha kutoa sehemu muhimu na za kawaida za uchi wa mwanamke na msichana pamoja na kutatiza shughuli za kawaida za miili ya wasichana na wanawake.

Matatizo yanayotokana na Ukeketaji mara moja ni kama:

- Uchungu mwingi
- Mshtuko
- Kutoka kwa damu
- Tetanasi/pepopunda ama sepsisi
- Kuziba kwa mkojo
- Vidonda kwenye sehemu ya uchi wa mwanamke au msichana

Athari za kiafya – za baadaye

Athari za Ukeketaji zitakazotokea baadaye ni kama:

- Maambukizo ya kibofu na mkondo wa mkojo ya kila mara(UTI)
- Uvimbe (uliojaa maji) na keloidi (makovu makubwa kupita kiasi)
- Kukosa kushika mimba na kuzaa
- Uwezekano mkubwa wa matatizo wakati wa kujifungua pamoja na kufa kwa mtoto
- Haja ya upasuaji baadaye
- Hedhi yenye uchungu au kuzuiliwa kwa hedhi
- Maambukizo ya VIRUSI VYA UKIMWI (VVU)

Ni (utamaduni) haramu

Ukeketaji ilipigwa marufuku kisheria nchini Kenya katika mwaka wa 2011.

Sheria inaharamisha kufanya ama kumfanyia mwengine ukeketaji au hata kumpeleka mtu ng'ambo kukeketwa.

Ni haramu pia kutoa nafasi kwa shughuli za Ukeketaji vile vile ni hatia kujua kufanyika kwa uhalifu huu na kukosa kuripoti.

Sheria inapiga marufuku kuwa na vifaa vinavyotumiwa kukeketa.

Sheria inapiga marufuku matusi dhidi ya wanawake au wasichana wasiokeketwa.

Wanaopatikana na hatia chini ya sheria hii wanaweza kufungwa kwa muda usiopungua miaka mitatu au kupigwa faini isiyopungua shilingi laki mbili ama zote.

Mtu akifa akikeketwa basi mkeketaji atafungwa maisha.

